# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI

# Bumbuli na mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi

**NA MWANDISHI WETU, BUMBULI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bumbuli ni miongoni mwa Halmashauri 11 za Mkoa wa Tanga. Halmashauri hiyo imetokana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Mwaka 2012 kama ilivyotangazwa katika gazeti la Serikali na kuanza rasmi mwezi February 2013.

Baada ya kumegwa eneo la jimbo la Bumbuli na kuanzishwa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli. Halmashauri hii ina tarafa 3, ambazo ni Soni, Mgwashi na Bumbuli, Kata 18, Vijiji 83 na Vitongoji 683, Halmashauri ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 708.

Mipaka ya Halmashauri kwa upande wa Kaskazini Halmashauri inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Magharibi, Kusini na Mashariki inapakana na Wilaya ya Korogwe. Shughuli kuu za kiuchumi za wananchi wa Bumbuli ni kilimo na zao kuu la biashara ni Chai.



**Mafanikio ya miradi iliyotekelezwa**

Akizungumzia mafanikio yake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Bw. George D. Haule anasema tangu kuanzishwa kwake rasmi mwaka 2013 Halmashauri imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Anasema miradi hiyo ni ile iliyopo katika sekta ya elimu, Afya, kilimo, Utawala, ufufuaji wa kiwanda cha chai Mponde na uhifadhi wa misitu ya jamii na Hifadhi, upimaji wa viwanja 241 katika eneo la Kwehangala na Soni.

"Kuongeza udahili wa wanafunzi kidato cha kwanza, awali na darasa la kwanza, ujenzi wa kituo kipya cha Afya milingano, kuboresha miundo mbinu ya vituo vya afya Mgwashi, na Tamota" anasema.

**MAFANIKIO HAYO YA SEKTA ELIMU KAMA IFUATAVYO**

| NA | MWAKA | MADARASA | MADAWATI | MATUNDU YA VYOO | NYUMBA | MAJI YA KUNAWIA MIKONO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2016/2017 | 2 | 60 | 0 | 0 | 0 |
| 2 | 2017/2018 | 2 | 3417 | 0 | 0 | 0 |
| 3 | 2018/2019 | 9 | 450 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | 2019/2020 | 15 | 540 | 42 | 2 | 0 |
| 5 | 2020/2021 | 16 | 480 | 72 | 0 | 0 |
| 6 | 2021/2022 | 8 | 540 | 16 | 0 | 2 |
| | **JUMLA** | **52** | **5487** | **130** | **2** | **2** |



**Miradi ya shule za sekondari**

Anasema Halmashauri imejenga vyumba vya madarasa 92 matundu ya vyoo 93, meza na viti vya wanafunzi 3680 pamoja na nyumba za walimu 5.

| MWAKA | MADARASA | VYOO MATUNDU | VYUMBA | MAABARA | BWENI | UKUMBI | MRADI WA MAJI SHULENI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013/2014 | 4 | 10 | 3 ( 1 i n 6) | 1 | | | |
| 2014/2015 | | 30 | | 1 | 2 | | |
| 2015/2016 | 4 | 10 | 1 | 1 | 2 | | |
| 2016/2017 | 6 | 10 | | | | | |
| 2017/2018 | | | 1 | | | | |
| 2018/2019 | | | | | | 1 | |
| 2019/2020 | 4 | 11 | | | | | 1 |
| 2020/2021 | 6 | 22 | | 7 | | | |
| 2021/2022 | 68 | | | 5 | | | 1 |
| **JUMLA** | 92 | 93 | 5 | 15 | 4 | 1 | 2 |

**MIRADI YA TOZO**

Ukamilishaji wa madarasa 3, darasa 1 shule ya Sekondari Mkaalie na madarasa 2 shule ya Sekondari kwamongo.

**MIRADI YA UVICO**

Ujenzi wa jumla ya madarasa 54 katika shule za Sekondari Baga 3, Bumbuli 2, Chai 2, Funta 3, Januari Makamba 2, Kizanda 2, Kizimba 2, Kwalei 2, Kwamongo 2, Kwehangala 2, Mahezangulu Makamba 2, Mayo 2, Mazumbai 3, Mbelei 3, Mbuzii 2, Mgwashi 2, Mibukwe 3, Mkaalie 2, **Mponde 2,** Msamaka 2, Soni 2, Tamota 2, Vugabazo 3 pamoja na Wena 2




**MAFANIKIO SEKTA AFYA KAMA IFUATAVYO**

**Miradi ya Afya**

Anasema Halmashauri imejenga kituo kipya cha afya Milingano na kuboresha vituo viwili vya Afya vya Mgwashi na Tamota pamoja na ukamilishaji wa Zahanati tisa za Kwemisambia, Kwadoe, Kihitu, Mziasaa, Kidundai, Lwandai, Kwanguruwe, Nkongoi, Kwendoghoi na Kwesine ambazo kila moja ilipata milioni hamsini (T.sh. 50,000,000.00) sawa na T.sh 450,000,000.00. kwa zahanati tisa, Halmashauri imeanza kujenga Hospitali ya Wilaya katika eneo la Kwehangala.





**UJENZI WA JENGO LA UTAWALA.**

Anasema Halmashauri inajenga jengo la utawala katika eneo la Kwehangala ambapo hadi sasa jengo hilo limefikia asilimia 81 ya kukamilika.


**Ufufuaji wa kiwanda cha usindikaji zao la chai Mponde**



**Miradi ya barabara**

Mkurugenzi Mtendaji Haule, anasema Halmashauri kupitia TARURA imeweza kuboresha barabara ambazo zinapitika kwa mwaka mzima kwa kiwango cha Moram na kujenga barabara ya Bumbuli Sokoni,

Anasema kuanzia stendi hadi hospitali ya Bumbuli Mission barabara ya kiwango cha lami kwa urefu wa kilomita 1 kwa Bumbuli na barabara ya Soni Mponde, kiwango cha lami kwa urefu wa kilomita moja na pia Mkandarasi yupo 'site' kwa ajili kuongeza kilomita moja ya lami katika barabara hiyo.



**MSITU WA BAGA**

Msitu huu upo katika kata ya Baga ambao unahifadhiwa na kutunzwa na Halmashauri kwa ajili ya chanzo cha maji ambayo yanatumika katika kata ya Baga, Bumbuli, Ngwashi na Mayo.

**MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA UTOAJI WA MIKOPO YA ASILIMIA 10 WAJASILIAMALI.**

Anasema kumekuwepo na ongezeko kwa kiasi cha utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kutokana na ukusanyaji wa mapato ya ndani ambayo kwa

mwaka wa fedha 2021/2022, ambapo Halmashauri hiyo imetoa mikopo kutokana na makusanyo kwa asilimia 98.

"Mapato haya ni yale yasiyofungiwa kwa mwaka yalikuwa 444.175,098.50 ambapo 10% yake ni 44,417,598.00 na kiasi kilichotolewa mikopo ni 44,040,278.00 kwa tofauti ya 377,320.00" anasema.

Anaongeza kwa kusema "Kukusanya marejesho ya mikopo na kutumia kiasi cha marejesho hayo kuwakopesha walengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, ambapo Halmashauri ilifanikiwa kukopesha marejesho yenye thamani ya TZS 34,300,000.00 katika vikundi vya wanawake, vijana.

"Mikopo imeongeza kipato cha wanavikundi na kupunguza utegemezi au umaskini kama walengwa wengi wanavyoshuhudia. Mikopo imepunguza matukio ya uhalifu kwani vijana wengi waliokuwa wanajihusisha na matukio ya uhalifu wamejengewa uwezo wa ujasiriamali na kuwa miongoni mwa wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani" anasema.

Haule anasema kumekuwa na ongezeko la mzunguko wa fedha. Serikali inapotoa mikopo ya asilimia 10 inaongeza mzunguko wa fedha mitaani. Wengi wa wanaopata mikopo ni miongoni mwa asilimia ya wakulima ambao mara baada ya kuvuna mazao wanakuwa hawana kazi na kubaki vijiweni.

"Mikopo hiyo imeongeza shughuli za kiuchumi (diversification of economic activities). Kuongezeka thamani kwa mazao ya mashambani kutokana na usindikaji wa matunda, mbogamboga, viungo mbalimbali kama Iliki, Chai, Miwa, Kahawa na Tangawizi" anasema.

Anasema "kupungua kwa upotevu wa mazao unaotokana na kusafirisha mazao ghafi, kupungua kwa gharama za usafirishaji wa mazao ghafi, kupungua kwa migogoro katika familia na jamii, elimu ya ujasiriamali imeongeze katika Jamii na Ujuzi wa kuandika maandiko ya miradi pamoja na kujua fursa zilizopo katika maendeo yao na jinsi ya kuziendeleza kibiashara kwa kuziboresha/ kuziongezea thamani na kujiongezea kipato, pia kuzitangazia masoko ya nje".

"Uchumi wa viwanda vidogo vidogo umekua kama mashine za kukoboa na kusaga nafaka, Ushonaji, Migahawa. Mabadiliko ya fikra kwenye Jamii (mindset changes) hasa kwa Wanawake Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa kuwa na Ujasiri wa kuwa na mahusiano ya karibu na Ofisi zao za Serikali za Mitaa" anasema.

Aidha, anasema serikali kutoa mikopo isiyokuwa na riba ni ishara ya upendo wa Serikali kwa wananchi wake na upendo kwa wanajamii pamoja na mahusiano mazuri na kujuana zaidi na kwa karibu kuongezeka wanapojiunga katika vikundi vya pamoja kiuchumi.

**CHANGAMOTO ZA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKOPO**

Anasema baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo kwa wakati kulingana na mikataba, huku vikundi vingine kuwa na mkopo zaidi ya mmoja (kukopa taasisi nyingine za fedha) na kupelekea kushindwa kurejesha ipasavyo.

"Siasa kuingizwa katika mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani, kutopata waombaji wa mkopo kwa uwiano wa 4:4: 2" anasema.

Utatuzi wa changamoto na mikakati ya Utoaji na urejeshaji wa mikopo

Anasema kuendelea kutoa elimu kwa wanavikundi juu ya matumizi lengwa ya mkopo, kuendelea

kushirikiana na shirikisho ya vyama vya watu wenye ulemavu (SHIVYAWATA) kwa lengo la kuwajulisha uwepo wa mikopo, taratibu za kupata mikopo hiyo na marejesho

Anasema "Kutangaza fursa za mikopo mara kwa mara katika jamii. Kutoa elimu ya ujasiriamali kabla na baada ya kupata mkopo katika makundi ya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu".

Hivyo, anasema agenda ya mikopo inajadiliwa katika ngazi za kamati za maendeleo ya kata (WDC), Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT), kamati ya Fedha na Uongozi pamoja na baraza la madiwani (Full Council)".

**MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA.**

Anasema Halmashauri inatarajia kutekeleza miradi ya kutoa huduma za afya kama Zahanati kwa kila kijiji na kupanua vituo vya Afya pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo imeanza kujengwa.

Mipango ya Halmashauri katika kuongeza mapato na uchumi katika pato la Taifa.

Anasema mipango ya Halmashauri katika kuongeza pato la Taifa ni kuhamasisha zaidi kilimo cha chai kutokana na kiwanda cha Chai Mponde kinafunguliwa, kuhamasisha kilimo cha Mkonge, uwekezaji katika mahoteli ya kitalii.

**FURSA ZA KIUWEKEZAJI ZINAZOPATIKANA**

Anasema fursa za uwekezaji kwa Halmashauri inatokana na mandhari yake ya Misitu inayofaa katika uwekezaji wa viwanda vya Chai, Mahotel ya kitalii, Viwanda vya Maji na juisi. Kilimo cha mbogamboga (nyanya) kwa kutumia "green house" na kilimo cha matunda (parachichi na matunda mengine)